**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*07 Februari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS MUSEVENI AFANYA ZIARA YA KIKAZI YA SIKU MOJA, NCHINI

Rais wa Jamhuri ya Uganda, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, leo amefanya ziara ya kikazi ya siku moja nchini Tanzania kwa mwaliko wa mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Viongozi hao walifanya mazungumzo ya pamoja ya pande mbili yaliyolenga kuimarisha uhusiano wa kindugu na kihistoria kati ya Tanzania na Uganda, pamoja na kuendeleza ajenda ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Katika mazungumzo yao, walisisitiza umuhimu wa kuharakisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati, ikiwemo Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (EACOP), miradi ya mabomba ya gesi na mafuta yaliyosafishwa, pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji na usafirishaji wa bidhaa kupitia Bandari za Dar es Salaam na Tanga.

Marais hao pia walikubaliana kuendelea kuimarisha matumizi ya miundombinu ya reli, barabara na usafiri wa majini katika Ziwa Victoria, ili kurahisisha biashara na kuongeza ushindani wa bidhaa za kikanda katika masoko ya kimataifa.

Katika eneo la biashara, walisisitiza dhamira ya kuendelea kuondoa vikwazo visivyo vya kikodi, kuboresha mazingira ya biashara, na kuimarisha soko la Afrika Mashariki kwa manufaa ya wananchi wa nchi wanachama.

Aidha, walijadili masuala ya usalama wa kikanda, amani katika Ukanda wa Maziwa Makuu, pamoja na ushirikiano katika majukwaa ya kimataifa na kikanda, ikiwemo Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Tanzania ilishukuru Uganda kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za pamoja katika masuala ya diplomasia na usalama.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia alimpongeza Rais Mteule Museveni kwa ushindi katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika nchini Uganda hivi karibuni, na pia kwa mchango wake katika kuimarisha mshikamano wa kikanda.

Kwa upande wake, Rais Museveni alisisitiza umuhimu wa kujenga uchumi wa uzalishaji, soko la pamoja, na mshikamano wa Afrika katika kukabiliana na changamoto za kimataifa. Viongozi hao walithibitisha dhamira yao ya kuendelea kushirikiana kwa karibu katika utekelezaji wa miradi ya pamoja, kwa lengo la kukuza ustawi wa wananchi wa Tanzania na Uganda, pamoja na kuchangia maendeleo endelevu ya Afrika Mashariki.

Rais Museveni alihitimisha ziara yake salama na kuondoka nchini kurejea nchini kwake Uganda.

**MAELEZO KWA MHARIRI**

Biashara kati ya Tanzania na Uganda imeendelea kukua, ambapo mauzo ya Tanzania kwenda Uganda mwaka 2025 yalifikia dola za Marekani **milioni 134.7**, huku uagizaji kutoka Uganda ukiwa dola **milioni 88.2**, na hivyo kuifanya Tanzania kuendelea kuwa na uwiano chanya wa biashara.

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (EACOP), unaounganisha Hoima (Uganda) na Tanga (Tanzania), ulikuwa umefikia asilimia **79** ya utekelezaji kufikia mwezi Januari, 2026 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2026.

Mradi huu, pamoja na matumizi ya Bandari za Dar es Salaam na Tanga kwa ajili ya usafirishaji wa mafuta na bidhaa, unaimarisha nafasi ya Tanzania kama lango kuu la biashara kwa Uganda na nchi nyingine zisizo na bandari.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu